# Jarida La MELI

TOLEO LA JUNI – SEPTEMBA 2021

WANAFUNZI WA NIT Waona Fursa Ujenzi Wa Meli.. UK. 2

MV BUTIAMA yasifiwa.. UK. 4

MSCL KUJIANDAA kusafirisha Tani 160 000 za Mtama UK. 7


# RAIS SAMIA AENDELEA KUMUENZI HAYATI JPM MIRADI YA MELI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akivuta na kukata utepe kuzindua chelezo ambacho kinatumika kutengeneza Meli mpya ya MV Mwanza katika sherehe zilizofanyika bandari ya Mwanza South mwezi Juni mwaka huu.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amesema mikataba mitano iliyosainiwa tarehe 15.6.2021 Mwanza ya ujenzi na ukarabati wa meli ni kazi nzuri ya kumuenzi Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ni mwanzilishi wa miradi hiyo.

Aliyasema hayo jijini Mwanza baada ya kuzindua chelezo, meli ya New Victoria 'Hapa Kazi Tu' na meli ya New Butiama 'Hapa Kazi Tu' pamoja na kushuhudia utiaji saini wa mikataba mitano ya ujenzi wa meli mpya nne na ukarabati wa meli ya zamani.

Rais Samia alisema anajisikia faraja kushuhudia kukamilika kwa ukarabati huo wa meli, kusainiwa kwa mikataba na kukamilika kwa ujenzi wa chelezo.

"Kama ingekuwa haijakamilika roho zetu zisingejisikia vizuri kwa sababu mwanzilishi wa miradi hii ameitwa na Mungu na ameitika, kama anatusikia bila shaka anafarijika," alisema Rais Samia.

Alisema ni dhamira ya serikali kuifanya Mwanza kuwa kituo kikubwa cha biashara kwa kuwa Mwanza iko kwenye ukanda wa mikoa wazalishaji wakubwa wa mazao wa chakula na biashara na mazao ya uvuvi, hivyo serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji na miundombinu laini ya kuboresha mawasiliano ya kimtandao.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli, Philemon Bagambilana alisema ukarabati wa meli hizo ulianza Januari 2019 kwa gharama ya Sh bilioni 27.6 na zilianza kufanya kazi tangu Agosti 16, mwaka jana.

Alisema meli ya New Victoria ina uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 200 za mizigo wakati New Butiama ina uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo.

"Meli ya New Victoria inafanya safari zake mara tatu kwa wiki kati ya Mwanza na Bukoba kupitia Bandari ya Kemondo, na meli ya New Butiama inafanya safari zake kila siku kati ya Mwanza na Nansio Ukerewe," alisema Bagambilana.

Aliongeza, "Ujenzi wa chelezo nao ulianza Januari 2019 kwa gharama ya shilingi bilioni 36.4, ni chelezo kikubwa kupita vyote katika Ziwa Victoria."

Alisema meli ya New Victoria ilitengenezwa mwaka 1960 na meli


*Inaendelea Ukurasa wa 2..*

# Wanafunzi wa NIT waona fursa ujenzi wa Meli nchini

Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Prof. Zacharia Mganilwa akiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi na walimu wa chuo hicho pamoja na watumishi wa MSCL katika eneo la ujenzo wa mradi wa meli ya MV Mwanza.

*Na Mwandishi Wetu*

Wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) wamejionea fursa mbalimbali zinazohusu muunganiko wa fani mbalimbali zinazofundishwa katika chuo hicho ili kufanikisha mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza unaosimamiwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

Wanafunzi hao walioongozwa na Mkuu wa Chuo hicho ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi MSCL, Prof. Zacharia Mganilwa katika ziara ya kujifunza kwa vitendo uendeshwaji na ujenzi wa meli, wanafunzi hao wamekiri kujifunza mengi ambayo hawakuyafahamu na hivyo kuhamasiska kushiriki katika miradi ya meli nchini.

Akizungumza muda mfupi baada ya kumaliza ziara hiyo mwanafunzi Gatu Vedastus alisema kuwa amefurahi kufika katika eneo la ujenzi wa meli ya MV Mwanza na kuona namna vijana wa kitanzania wanavyohusika kwa asilimia kubwa katika ukamilifu wa meli hiyo.

"Katika ziara yetu tumekuja watu wa kozi tofauti, kuna watu wa waliosomea 'Electrical Engineering' (uhandisi wa umeme), 'Telecommunication' (Mawasiliano ya Simu, 'Automobile' (magari), 'Mechanical Engineering (uhandisi mitambo), wote hao tumekuja hapa kujifunza na kuangalia ujenzi wa meli, hatupo hapa kujifunza tu, pia inatupa moyo na sisi pia, kama taarifa tuliopewa hapo kuwa wahandisi wanaoshughulika na ujenzi ni vijana wa hapa hapa Tanzania, hicho kitu mimi kimenihamasisha sana, naamini nami siku moja nitakuwa mjenzi wa Meli."

Kwa upande wake Prof. Mganilwa alisema kuwa wanafunzi hao wamejionea uhalisia wa kile wanachokisoma darasani na kuongea kuwa lengo la taaluma hizi za uhandisi ni kutatua matatizo katika sekta za usafirishaji nchini.

"Wamesoma kwa nadharia mwaka mzima leo hii wametembelea ujenzi wa meli, naamini yale waliyoyasoma kwenye nadharia leo wanayaona yanafanyika na kwasababu hii sekta ya ujenzi wa meli kwa nchi ya Tanzania ni eneo ambalo tukiweza kupata rasilimali watu wa kutosha itaweza kutoa mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi hii," alisema.

# RAIS SAMIA AENDELEA KUMUENZI HAYATI JPM...

*...inatoka uk. 1*

ya New.... .....Butiama ni ya mwaka 1980.

Kuhusu mikataba mitano iliyosainiwa, alisema mkataba wa kwanza ulihusu ujenzi wa meli mpya katika Bahari ya Hindi kwa kulenga soko la Comoro na mkataba wa pili unahusu ujenzi wa meli mpya ya mizigo katika Ziwa Victoria itakayokuwa na uwezo wa kubeba tani 3,000 za mizigo kwa kulenga ujio wa Reli ya Kisasa (SGR).

Mingine ni ya ujenzi wa meli mpya ya mizigo katika Ziwa Tanganyika; wa nne ni ujenzi wa meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo, na mkataba wa tano ulihusu ukarabati wa meli ya MV Umoja yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na pia ina reli ndani yake.

Bagambilana alisema miradi yote hiyo itagharimu Sh bilioni 438.8.

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akizindua Chelezo ambacho kinatumika kutengeneza Meli mpya ya MV Mwanza.*

# WAFANYABIASHARA BUKOBA WAZUNG--UMZIA MAFANIKIO YA NEW VICTORIA.

*Na Mwandishi wetu*

Umoja wa Wafanyabiashara Soko Kuu la Wafanyabiashara Manispaa ya Bukoba wameushukuru Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano uliokuwa chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutimiza ahadi ya kuikarabati meli ya MV Victoria na hatimae kuwafungulia fursa ya kufanya biashara na hatimae kuwaongezea kipato na kuinua uchumi wao.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wa manispaa hiyo, Katibu wa Wafanyabiashara wa Soko hilo David Damian alisema kuwa kwa takriban miaka sita tangu kusimama kwa huduma ya meli hiyo wafanyabiashara hao wamekuwa wakipata tabu kusafirisha mazao yao kwa njia ya barabara ambayo inatumia gharama kubwa na kujiweka katika hatari ya kupoteza mzigo au kufika kwa kuchelewa kutokana na vyombo hivyo kutokuwa vya uhakika.

Akizungumza na MSCL mjini Bukoba, David alisema kuwa uchumi wa wafanyabiashara umekuwa baada ya mwaka mmoja tangu kuanza kwa huduma za meli hiyo na kuongeza kuwa hali hiyo imesababishwa na unafuu wa usafiri na usafirishaji wa mazao ya biashara hasa ndizi na maparachichi yanayolimwa kwa wingi katika mkoa wa Kagera.

"Mimi binafsi na kwa niaba ya wafanyabiashara wa Bukoba hususan wafanyabiashara wa ndizi, nasema tumenufaika sana na ujio wa meli, kwetu meli ni mkombozi, kwasababu tangu meli ianze takriban mwaka sasa, tumeona umuhimu wa meli kama tulivyokuwa nao awali, meli hii ni kiunganishi kikubwa kati yetu sisi, Mwanza na mikoa mingine ya Jirani, kwetu sisi meli ni fursa,"

"Nipende kumshukuru Hayati Rais aliyetutangulia aliona umuhimu wa meli kwasababu imekaa takriban miaka sita na kitu, hatuna meli, na kipindi hicho sisi uchumi wetu wa Bukoba haukuwa mzuri kwasababu kiunganishi kikubwa cha biashara ni meli, tunaposema meli sio kiunganishi tu, hata katika suala la bei za usafiri na usafirishaji kunaleta bei nafuu sana, ukipata faida unakuwa na uhakika sana, kuliko kusafiria magari makubwa (malori) ambayo gharama zake za kusafiria zinakuwa kubwa."

Meli ya New Victoria "Hapa Kazi Tu" ilifanya safari yake ya mwisho tarehe 18.12.2014 na kuongeza ugumu wa usafiri wa ziwani tangu kuzama kwa meli ya MV Bukoba tarehe 21.5.1996, lakini baada ya ukarabati mkubwa uliofanywa katika meli ya MV Victoria na kupelekea kubadilishwa jina la meli hiyo na kuitwa New Victoria kumesaidia usafiri katika ziwa hilo kuimarika na kuleta ahueni kwa wananchi na wafanyabiashara wa mkoa wa Kagera wanaosafirisha mazao zao kwenda Mwanza.

Wakati akielezea hali ilivyokuwa kipindi ambacho meli hiyo iliposimama kutoa huduma David alisema kuwa kabla ya meli hiyo kuanza tena kufanya kazi wimbi la usafirishaji wa mazao hayo halikuwa kubwa kama hivi sasa ambapo meli hiyo hubeba mzigo mkubwa ukilinganisha na usafiri wa magari.

"Nasema awali hali haikuwa nzuri kwasababu, ukiangalia uwezo wa ubebaji wa mizigo wa meli na ubebaji wa mizigo wa gari za kawaida unaona tofauti kubwa iliyopo, lakini pia nimeongelea suala la bei, kwenye meli kuna unafuu zaidi ambapo sisi wafanyabiashara unaona bora usafirishe na meli unapata faida kuliko kusafirisha kwa magari, lakini pia magari yanachangamoto kubwa kwa upande wa ndizi na matunda, kuna uwezekano wa kufika kati kati hapo mambo yakaharibika na uwezekano wa kupata hasara ukawa mkubwa,"

"Namshukuru sana Mungu aliyewapa viongozi wetu maono wakafufua maeli hiyo."

Meli ya New Victoria "Hapa Kazi Tu" inasafirisha tani moja ya mzigo kwa Shilingi 27,000/= wakati kwa usafiri wa malori, mfanyabiashara hutumia shilingi 80,000/= hadi Shilingi 120,000 kwa tani.

Katika kuhakikisha meli hiyo inakuwa ya kisasa miongoni mwa marekebisho yaliyofanyika ni kuondoa mfumo wa analojia wa uendeshaji wa meli na kuweka mfumo wa digitali unaopelekea meli hiyo kuwa na hisia pindi inapokaribia kukumbana na kikwazo ziwani na hivyo kuchukua hatua stahiki ikiwemo kusimama ili kuepusha ajali.

Katika upande wa kuongeza ajira, wabeba mizigo ni kundi lingine linalokiri kupata ukombozi kutokana na safari za meli kuanza wakisema walipoteza fursa ya kiuchumi kwa muda mrefu tangu usafiri huo uliposimama.

Tangu tarehe 16.8.2021 mpaka tarehe 31.5.2021, Meli ya New Victoria "Hapa Kazi Tu" imesafirisha abiria 140,664 pamoja na tani 15,102 za mizigo.

Meli ya New Victoria "Hapa Kazi Tu" ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Magufuli aliyoitoa

*Wafanyabiashara wa ndizi wilayani Bukoba wakiendelea na shughuli za kuuondosha mzigo wa ndizi uliopakuliwa kutoka kwenye meli ya New Victoria kwenye bandari ya Mwanza kaskazini*

# New Butiama Yasifiwa Kwa Kuzingatia Muda

*Na Mwandishi Wetu*

"Binafsi naweza nikasema kwamba na- ridhika na huduma yao, kwanza kwa wafanyakazi waliopo ni wakarimu, ni watu wanaojua kujali kwa tatizo la mtu yeyote yule bila ya kujali mazingira ya mtu husika, pili unapokuwa unasafiri nah ii meli unauwezo wa kupangilia muda wako kwamba nataka nifike kwa muda fulani na nataka nifanye shughuli zangu kwa muda ule, nirudi na unafika kwa muda muafaka, kwa upande wa changamoto mi binafsi sijawahi kuona."

Hayo ni maneno ya Mangoli Paulo, mmoja wa abiria anayetumia usafiri wa meli ya New Butiama katika Ziwa Victoria kutoka Mwanza kwenda Ukerewe na Kurudi ambaye amesifu huduma bora anayoipata kwa kutumia meli hiyo inayomwezesha kufanikisha shughuli zake kwa wakati.

Aidha, abiria huyo amewataka wafanyakazi wa meli hiyo na kampuni kwa jumla kutobweteka na sifa hizo na kuwapelekea kutoa huduma zitakazowakwaza wateja na hatimae kuihama meli hiyo.

Naye Jackson Malebezeja anayetumia usafiri huo kila siku za ljumaa na Jumatatu, amesifu huduma zinazotolewa kuanzia sehemu ya kukata tiketi hadi kufika kukaa kwenye siti na kupatiwa elimu ya kujiokoa endapo kutatokea shida yoyote katikati ya maji.

"Unakuta wengine hatujui hatuna elimu ya ubaharia, lakini wanakuelekeza kama itatokea tatizo unaweza ukajiokoa hivi na unatakiwa kufanya hivi, kwahiyo wanakupa na elimu ya kujiokoa pia halafu na ule muda wa kufika kwasababu ukikaa sana masaa manne, matano unachoka sana, unaweza ukachukia hata usafiri kwahiyo kwa kuwahi kwao mi naupenda sana usafiri wa New Butiama na Mungu aendelee kuibariki iwepo siku zote," Alisema.

Katika kusisitiza uzingatiaji wa muda kwa meli ya New Butiama abiria Grace Buyanza alifananisha uzingatiaji wa muda kwa meli hiyo ya serikali na meli inayoendeshwa na mtu binafsi kwa kusema kuwa New Butiama inazingatia zaidi mud ana hivyo kukuokolea muda

"Butiama inakuokolea muda wako, unafika kwa muda mchache, haina kero yoyote kwakweli kwangu mimi binafsi, ukiangalia hata upande wa kuchaji simu, unaweza kuchaji simu yako, unatulia, unasafiri vizuri, nimeupenda kwakweli, ni usafiri mzuri wa uhakika na unaoaminika, kwasababu unaweza ukatoka Ukerewe kuja Mwanza ukatumia muda mchache tofauti na meli nyingine."

Hayo yamesemwa na abiria wa meli ya New Butiama baada ya meli hiyo kutimiza mwaka mmoja tangu kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuanza kuwahudumia wananchi tarehe 16.8.2020 kwa safari za kutoka Mwanza kwenda Ukerewe na kurudi.

*Abiria wa MV Butiama, Mangoli Paulo, akitoa maoni yake baada ya kusafiri na Meli hiyo kutoka Mwanza kwenda Ukerewe (Kwenda na Kurudi) mbele ya Meli Yetu TV*

Timu iliyoongozana na Msanii Nandy katika tamasha la muziki la Nandy Festival wakipata Chakula katika Mgahawa wa Burigi – Chato uliopo ndani ya Meli ya New Victoria mara baada ya kumaliza ziara ya kutembelea meli hiyo.

Wasanii mbalimbali walioshiriki katika Tamasha la Nandy Festival wakiongozwa na Msanii Nandy wakiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Philemon Bagambilana pamoja na watumishi wengine wa MSCL

Msanii Nandy akiwa katika picha ya pamoja na manahodha wa meli ya New Victoria pamoja na New Butiama wakati msanii huyo alipotembelea meli ya New Victoria mapema mwezi wa Saba, 202.

# MSCL yatoa sababu tatu kusitisha kwa muda safari za meli za New Victoria na New Butiama

*Na Mwandishi Wetu*

Uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) umewatoa hofu abiria na wafanyabiashara mbalimbali wanaosadfirisha mizigo yao kwa njia ya maji kuhusu kusimama kwa muda kwa safari za meli ya New Victoria na New Butiama zinazotoa huduma katika Ziwa Victoria.

Akitaja sababu za kusitisha safari hizo Kaimu Afisa Mtendaji wa MSCL Mhandisi Abel Gwanafyo alisema kuwa meli ya New Victoria itasitisha safari zake kwa muda wa wiki mbili huku meli ya New Butiama itasitisha safari zake kwa muda wa siku nane ambapo zitapandishwa katika chelezo ili kufanyiwa uchunguzi baada ya kutoa huduma kwa muda wa mwaka mmoja.

Baadhi ya Wafanyabiashara wa ndizi wanaosafrisha mizigo yao kutoka Mkoani Kagera kwenda Mwanza kwa kutumia meli ya New Victoria "Hapa Kazi tu" wakiwa wameshusha mizigo yao muda mfupi baada ya meli hiyo kutia nanga Bandari ya Mwanza Kaskazini.

"Tunazipandisha kwasababu za kitaalamu, meli inapofanya kazi ndani ya maji ina muda wake wa kufanya kazi ikiwa chini ya mamlaka inayodhibiti vyombo vya majini, sasa meli hizo mbili zimemaliza muda wake wa mwaka mmoja tangu zianze kufanya kazi na zinapofanya kazi kinatolewa cheti cha ubora ambacho hudumu kwa mwaka mmoja, kwahiyo unalazimika upande kwenye chelezo ili kuchunguza kuona kama ubora bado upo kama ulivyokuwa awali, kwahiyo chombo hicho kinapanda kikaguliwe ili kithibitishwe tena na mamlaka husika yaani TASAC kama kina ubora ule ule ili kiendelee tena kufanya kazi,"

Aidha alifafanua kuwa meli hizo zilifanyiwa ukarabati mkubwa ulioghrimu Shilingi bilioni 27.6, ukarabati uliotekelezwa na Mkandarasi KTMI Co. Ltd ya Korea Kusini na hivyo kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja cha matazamio (Defect liability period) na kuongeza kiuwa mapungufu madogo madogo yaliyojitokeza katika kipindi hicho ni muhimu kurekebishwa baada ya kupanda kwenye chelezo

"La tatu ni kiufundi, kwamba 'tear and wear' (kuchakaa) kwa vyombo vyetu hivi vinavyosafiri majini, mwili wa meli unaozama majini huwezi ukauona kwa macho, lazima upande kwenye chelezo, natoa mfano mzuri kwamba wewe unaendesha gari lako kwamba tairi likichomoka si unakwenda gereji sasa gereji ya meli ni chelezo kwamba eneo la chini huwezi kuliona kwa macho kwamba unaweza kutumia njia nyingine kama wazamiaji lakini hawawezi kuchunguza kwa uhuru zaidi kuliko meli ikipanda kwenye chelezo,"

Mhandisi Gwanafyo alisema kuwa hayo yote yanafanyika ili kutimiza msemo wa wahenga kuwa kinga ni bora kuliko kuponya, na hivyo kila baada ya mwaka lazima vyombo hivyo vichunguzwe ili kuvijua hali yake na mapungufu yakionekana yarekebishwe kwaajili ya usalama wa abiria, mizigo na chombo chenyewe.

Kwa upande wake Meneja Masoko wa MSCL Anselm Namala alielezea mpango wa kampuni katika kuboresha huduma zinazopatikana ndani ya meli ikiwemo sehemu ya burudani ya mziki wa bendi kwa kuongeza mwanamuziki mwingine wa kike tofauti na sasa kuwepo na wa kiume pekee, huduma ya chakula pamoja na kufanyia kazi changamoto mbalimbali zinazowasilishwa na abiria kwa kampuni.

"Usafiri tunataka iwe ni sehemu ya starehe, mtu asisafiri kwa kusikitika na kupata changamoto, kwahiyo tunatumia pia hii nafasi ya 'docking' (meli kupandishwa kwenye chelezo) kutatua changamoto ambazo wateja wametuletea na kuzifanyia kazi ili watakapoanza tena kusafiri wasipate shida yoyote, tunataka mtu akisafiri nasi asitusahau,"

# MSCL YAJIANDAA KUSAFIRISHA TANI 160,000 ZA MTAMA

*Na Mwandishi Wetu*

Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari (TPA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) wamekutana na Shirika la Chakula Duniani (WFP) na kufanya tathmini ya uwezekano wa kusafirisha tani zaidi ya 160,000 za mtama kupitia ushoronba wa kati ili kufikisha shehena hiyo nchini Sudani Kusini pamoja na Somalia.

*Wawakilishi kutoka MSCL, TPA, TRC na WFP wakikagua moja ya miundombinu itakayotumika katika kusafirisha tani zaidi ya 160,000 kutoka Tanzania kuelekea Sudani Kusini*

Taasisi hizo ambazo zilikutana katika ofisi za makao makuu ya MSCL Jijini Mwanza, waliweza pia kutembelea miundombinu inayomilikiwa na taasisi hizo ili kujiridhisha na ubora wa utendaji kazi kabla ya zoezi hilo kuanza jambo litakalotoa fursa taasisi za serikali pamoja na wakulima wa zao la mtama nchini.

Akizungumza baada ya ziara hiyo Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na manunuzi wa WFP Jose Ferrao amesema kuwa WFP ina ndoto ya kusafirisha tani 160,000 kuanzia miaka miwili au mitatu ijayo kwenda katika nchi za Sudani kusini na Somalia.

"Tunataka kuhakikisha kwamba ndoto waliyonayo WFP ya kusafirisha tani 160,000kwa mwaka inafikiwa katika miaka miwili au mitatu ijayo, hilo ndio lengo kubwa na tunaamini tunaweza kufanikiwa, hatufanyi kazi na TRC, TPA na MSCL pekee bali tunahakikisha pia wakulima wetu wanazalisha mtama wa kutosha ili kuyafikia malengo pamoja na kusafirisha kwa wakati."

Kwa upande wake Mkuu wa kitengo cha Usafirishaji WFP Mahamudu Mabuyu amesema kuwa shehena hiyo inayotakiwa kusafirishwa ni fursa kwa wakulima wetu wa mtama nchini lakini pia ni fursa kwa taasisi zetu za serikali katika kuboresha miundombinu na hivyo kuleta chachu kwa wadau wengine kuweza kutumia ushoroba huu.

"WFP tumekuwa wadau wakubwa wa huu ushoroba na lengo letu kubwa ni kuona huu ushoroba unaendelea, sisi tumekuwa kama chachu tu, tunaanzisha ili tuite wadau wengine wajiunge, tunategemea kwamba huu uwe ni mwanzo tu, Sudan Kusini wanahitaji tani karibu 165,000 ya mtama kwa mwaka na sisi tumekuwa tukipata kwa robo angalau tani 20,000 ya kununua Tanzania lakini haifiki kwasababu uzalishaji ni mdogo lakini tunashukuru uzalishaji unaanza kuongezeka, tunataka hata kama tusifikie tani 165,000 basi tufike hata nusu, kwahiyo hii ni fursa kwa wakulima wetu watanzania, fursa kwa TPA, MSCL na TRC

''Tunaiona fursa sasa kwa wakulima wa ndani hapa nchini kutumia fursa hii kulima zao la mtama kwani tunahitaji takribani tani laki moja na sitini elfu kwa mwaka ili kusafirisha na kupeleka nchi za Sudani ya Kusini na Somalia''

Akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa MSCL, Meneja Masoko na Biashara Anselm Namala alisema kuwa hivi kampuni inamipango ya kukarabati meli ya MV Umoja yenye uwezo wa kubeba kontena 19 pamoja na ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba kontena 49 ili kuweza kukidhi mahitaji ya mzigo huo siku zijazo.

Kwa upande wa TPA na TRC walitoa neno la shukurani ili na kuahidi kutoa ushirikiano katika zoezi hilo huku wakibainisha mikakati mbalimbali ya kuimarisha miundombinu iliyopo ili kuweza kukidhi kutimiza ndoto hiyo.

Kaimu Mhandisi wa Kampuni Mhandisi Abel Gwanafyo amesema kuwa taratibu za kuanza utekeleaji wa Ukarabati wa MV Umoja zimekamilika ambapo Mkandarasi S/M Solution kutoka nchini Korea ya kusini ndiye atakayehusika na ukarabati wa meli hiyo utakaochukua muda wa miezi 13 wakati mradi wa Ujenzi wa meli mpya utafanywa na Mkandarasi M/S Yutek kutoka nchini Uturuki.

*Wawakilishi kutoka MSCL, TPA, TRC na WFP wakiwa katika picha ya pamoja muda mfupi baada ya mkutano wa kujadili namna ya kusafirisha tani zaidi ya 160,000 kutoka Tanzania kuelekea Sudani kusini.*

# MV CLARIAS TAYARI KURUDI ZIWANI KUWAHUDUMIA WANANCHI

*Na Mwandishi Wetu*

Baada ya kusimama kutoa huduma kwa muda wa takriban miezi kumi, hatimaye meli ya MV Clarias inaelekea Ziwa Victoria.

Meli hiyo inarudi kutoa huduma baada ya kumalizika kwa ukarabati mdogo uliofanyika katika meli hiyo ili kuweza kuwahudumia wananchi kwa uhakika.

*MV Clarias ikiwa tayari kwa ajili ya kuanza safari baada ya kufanyiwa marekebisho*

kurudi ziwani kutoa huduma kwa wananchi wanaoishi katika visiwa kadhaa vya

Utaratibu huu wa kuifanyia meli matengenezo kila baada ya mwaka mmoja wa utoaji

wa huduma unaisaidia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuepusha ajali zinazosababishwa na uharibifu wa chombo cha kusafiria na kupata cheti cha ubora kinachotolewa na Shirika la Uwakala wa Meli nchini (TASAC).

Akizungumza wakati wa kuishusha meli hiyo kutoka kwenye chelezo inayoelea, Kaimu Mhandisi Mkuu wa MSCL Mhandisi Abel Gwanafyo amesema kuwa baada ya meli hiyo kupandishwa kwenye Chelezo mwezi April,2021, meli hiyo ilikaguliwa sehemu ya chini ya mwili pamoja na kufanyiwa marekebisho.

"Tulikuta sehemu kubwa ya chuma imepungua ubora ikatulazimu kuitoa na kuweka chuma chenye ubora zaidi lakini pia kuna sehemu awali walitumia Seruji kwenye chuma tumeiondoa sababu kitaalamu haikubaliki na sehemu zote hizo kulikuwa na matundu baada ya kuondoa saruji na matundu hayo tumeyafanyia kazi'', alieleza.

Miongoni mwa marekebisho yaliyofanyika katika sehemu ya chini ya mwili wa meli hiyo ni pamoja na kuwekwa mabamba mapya (plates), propela shafti pamoja na vilinda mwili (Zink Anord) na hivyo kubakisha maeneo machache ya kurekebisha ndani ya meli wakati meli ikiwa nje ya chelezo.

Meli hii inatarajiwa kurejea kutoa huduma hivi karibuni ikiwa na muonekano mpya.

*Meli ya MV Clarias ikirudishwa majini baada ya kufanyiwa marekebisho*

SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

- CEO
- AFISA MASOKO
- SAFETY AND MARINE TRANSPORTATION OFFICER
- HUMAN RESOURCE OFFICER
- CAPTAIN

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

MELI YETU

JUNI – SEPT 2021

# VIJANA WANAOJENGA MELI WATA--MBULIWE RASMI – DKT. DIALO

*Na Mwandishi Wetu*

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza Dkt. Anthony Dialo ameishauri menejimenti ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuona uwezekano wa kuwatambua rasmi vijana wanaoshiriki katika mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza katika bandari ya kusini, mkoani Mwanza.

Amesema kuwa kwa kufanya hivyo kutawarahisishia vijana hao kupata kazi za ujenzi wa meli hasa kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa na MSCL katika Ziwa Tanganyika, Victoria na Bahari ya Hindi.

"Najua sasa hivi wanatumia leseni zao, kwasababu kujenga meli duniani, lazima uwatumie wachomeaji waliosajiliwa, inamaana waliosomea kuchoma, lakini sasa leseni zao tunazitumia kwaajili ya kuwapa hawa vijana uelewa, sasa sijui MSCL mtafanyaje, maana wengine watakuwa wabobezi kweli kweli baada ya mradi kuisha, muwatafutie utaratibu wa kutambulika," Alisisitiza.

> **Mpaka sasa huu mradi umeshatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zaidi ya 1500**
>
> **Mh. Dialo**

Aliongeza kuwa elimu wanayopata vijana hao katika mradi huo itatumika kuisambaza kwa vijana wengine katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa meli katika maeneo tofauti ya nchi.

Ushauri huo umetolewa wakati Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Mwanza ilipofanya ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza wenye thamani ya Shilingi Bilioni 89.76 unaotekelezwa na Mkandarasi Gas Entec kwa ushirikiano na Kaang Nam zote za nchini Korea Kusini pamoja na SUMA JKT.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo Kaimu Mtendaji Mkuu wa MSCL Philemon Bagambilana alibainisha kuwa mradi huo umeajiri karibu asilimia 90 ya watanzania, huku wengi wao wakiwa ni vijana

*Meneja wa Mradi wa Meli Mpya ya MV Mwanza Vitus Mapunda (Kushoto) akitoa maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa meli hiyo kwa kamati ya Siasa ya CCM mkoa wa Mwanza iliyoongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo Dkt. Anthony Dialo (aliyeshika kiuno)*

"Mpaka sasa huu mradi umeshatoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kama vile mama ntilie zaidi ya 1500, na kuna vijana wasiopungua 200 wakitanzania wanaendelea na kazi kwenye eneo hili, wanachuo kama Chuo cha Usafirishaji NIT na Chuo cha Mabaharia Dar es salaam (DMI), wamepata fursa ya kufanya mafunzo yao kwa vitendo, kwahiyo imewasaidia kupata utaalamu, kwasababu ni meli ambayo inaundwa kuanzia mwanzo mpaka mwisho."

Mradi wa meli ya MV Mwanza ukikamilika utakuwa na uwezo wa kubeba tani 400 za mizigo, Abiria 1200, magari makubwa matatu na madogo 20, daraja la uchumi litabeba abiria 834, Daraja la Biashara abiria 200, daraja la kwanza abiria 100, sehemu ya watu washuhuri ni abiria 4, na sehemu kwaajili ya viongozi wenye hadhi ya kitaifa ni abiria 2.

*Meneja wa Mradi wa ujenzi wa Meli Mpya ya MV Mwanza Vitus Mapunda akiwaonesha wajumbe wa kamati ya siasa ya CCM Mkoa wa Mwanza maeneo yaliyofanyiwa kazi katika kipindi cha miezi miwili (hayapo pichani)*

**KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL)**

BANDARI YA MWANZA KASKAZINI, JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA, Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz Tovuti: www.mscl.co.tz

Kampuni ya Huduma za Meli | MSCLtz | mscltz | Meli TV

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI NCHINI